SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

SERA YA DIASPORA YA ZANZIBAR

2017

DIBAJI

Sera ya Diaspora ya Zanzibar inafafanua misingi ya kufaidika na michango ya Wanadiaspora wa Zanzibar kwa maendeleo ya Zanzibar kiuchumi na kijamii, wakati huo huo inaweka wazi mahitaji yao kwa kuweka utaratibu mzuri utakaosaidia kujenga uaminifu na utakaowavutia Wanadiaspora hao kuimarisha mahusiano na Nchi yao ya asili.

Kazi ya kuandaa Sera hii ilifanywa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (ORMBLM), kupitia vikao vya kukusanya maoni kutoka kwa Wanadiaspora wenyewe na kupata mapendekezo muhimu yaliyosaidia katika kutengeneza Sera hii. Aidha, mchakato wa kutaarisha Sera hii uliendelea kwa kufanya mapitio ya nyaraka rasmi na zisizorasmi zilizochapishwa na ambazo hazikuchapishwa zenye uhusiano wa moja kwa moja na Sera hii. Vile vile, majadiliano yaliyofanywa katika makundi maalumu, watu mbali mbali mashuhuri Serikalini, Taasisi Binafsi, Asasi za Kiraia, Wanadiaspora waliorejea nyumbani na hatimae kwa wanachama wa Jumuiya za Diaspora.

Masuala ya Diaspora yana umuhimu mkubwa na yanafahamika kuwa ni fursa muhimu katika maendeleo ya nchi. Hii ndio sababu iliyopelekea kuliingiza suala hili katika Sera na hatimae kuingizwa rasmi katika mikakati ya maendeleo ya Zanzibar. Sera hii imeweka Dira, Dhamira, malengo na muundo wa kitaasisi uliowazi na utakaowawezesha Diaspora kwa ufanisi mkubwa kuchangia maendeleo ya nchi yao ya asili. Serikali imejizatiti kuhakikisha kuwa Sera ya Diaspora ya Zanzibar inatekelezwa kwa ufanisi na inatoa matokeo yaliyokusudiwa.

Katika kuhakikisha utekelezaji wa Sera ya Diaspora ya Zanzibar unafanikiwa, uwekaji wa mazingira mazuri na uanzishaji mfumo bora zaidi wa kisheria katika uendeshaji wa suala la

Diaspora ni jambo la msingi. Kwa kuzingatia hilo, Serikali itahakikisha Idara inayosimamia Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi inafanya kazi kwa kushirikiana na wadau wengine katika kufuata taratibu zilizowekwa na Sera. Muda uliopangwa kufikia lengo unahitaji kuchungwa vizuri na kuwekewa miundo mbinu mizuri kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini.

Pamoja na Utangulizi, Sera hii kwa ujumla ina sehemu kuu tano; Sehemu ya kwanza inaelezea historia na hali halisi ya Diaspora wa Zanzibar, Sehemu ya pili ya Sera inafafanua Diaspora wa Zanzibar, Dira, Dhamira, Tunu na Miongozo ya Sera; wakati Sehemu ya tatu inaonesha Mantiki na Malengo ya Sera. Sehemu ya nne inatoa Matamko ya Kisera na Mikakati ya utekelezaji na mwisho, Sehemu ya tano inaelezea kazi na majukumu ya Taasisi mbali mbali ambazo ni wahusika katika utekelezaji wa Sera hii na mapendekezo ya taratibu za ufuatiliaji na tathmini yake.

ORMBLM inawashukuru Wahusika wote, Taasisi na watu binafsi waliochangia katika kuifanikisha Sera hii ya Diaspora Zanzibar. Matarajio yetu ni kwamba matokeo ya utekelezaji wa Sera hii yatasaidia katika kuonesha umuhimu wa Wanadiaspora katika kuchangia maendeleo ya Nchi yao na vile vile kuimarisha ukuaji na ustawi wa Wanadiaspora.

ISSA HAJI USSI GAVU
WAZIRI WA NCHI,
OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI ZANZIBAR

YALIYOMO

DIBAJI	ii
YALIYOMO	iv
ORODHA YA VIFUPISHO NA MANENO	vi
SURA YA KWANZA	**1**
HISTORIA NA HALI HALISI YA DIASPORA ZANZIBAR	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Historia, Watu na Uchumi wa Zanzibar	3
1.3 Hali ya Diaspora Kimataifa	4
1.4 Zanzibar na Hali ya Diaspora	5
SURA YA PILI	**9**
MAANA YA DIASPORA WA ZANZIBAR, DIRA NA DHAMIRA YA SERA	9
2.1 Maana ya Diaspora	9
2.2 Miongozo ya Kanuni za Sera	10
2.3 Dira ya Sera	10
2.4 Dhamira ya Sera	10
SURA YA TATU	**11**
HAJA YA KUWEPO KWA SERA NA MALENGO YAKE	11
3.1 Haja ya Kuwepo kwa Sera ya Diaspora	11
3.2 Malengo ya Sera ya Diaspora	11
SURA YA NNE	**13**
HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA	13
4.1 Kuijengea uwezo Idara inayoshughulikia masuala ya Diaspora	13
4.2 Usimamizi wa Taarifa zinazohusu Diaspora	13
4.3 Kuwashirikisha Wanadiaspora	14
4.4 Kutumia Taaluma na Ujuzi wa Wanadiaspora kwa maendeleo ya Nchi	15

4.5 Utumaji Fedha kutoka kwa Wanadiaspora 16
4.6 Diaspora na Biashara na Uwekezaji Vitega Uchumi 17
4.7 Diaspora na Utalii 18
4.8 Diaspora na Misaada ya Kijamii 18

SURA YA TANO 20
WAJIBU, MAJUKUMU YA KITAASISI, TATHMINI NA UFUATILIAJI 20
5.1 Mfumo wa Uratibu 20
5.2 Wajibu na Majukumu ya Kitaasisi 20
5.2.1 Idara inayoshughulikia Diaspora 21
5.2.2 Jukwaa la Diaspora 21
5.2.3 Majukumu ya Wizara, Idara na Mawakala wa Serikali na Wahusika wengine 22
5.2.4 Tume ya Mipango 22
5.2.5 Mamlaka Kukuza Uwekezaji Zanzibar 22
5.2.6 Benki Kuu, Benki za Biashara na Taasisi za Fedha 23
5.2.7 Kamisheni ya Utalii 23
5.2.8 Jumuiya za Wanadiaspora wa Zanzibar 23
5.2.9 Washirika wa Maendeleo na Taasisi nyengine za Kimataifa 24
5.2.10 Vyombo vya Habari 24
5.2.11 Ofisi za Kibalozi 24
5.2.12 Idara ya Uhamiaji 24
5.3 Ufuatiliaji na Tathmini 25

ORODHA YA VIFUPISHO NA MANENO

CRDB	Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini
FDI	Vitega Uchumi vya moja kwa moja kutoka Nje ya Nchi
IFAD	Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo
ILO	Shirika la Kazi Duniani
IMF	Shirika la Fedha Duniani
MKUZA	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar
ODA	Misaada Rasmi ya Maendeleo
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TOKTEN	Usafirishaji wa Taaluma kupitia Mitandao ya Wataalamu
UNDESA	Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Maendeleo ya Uchumi na Kijamii
UNDP	Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
UNESCO	Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa
US$	Dola za Kimarekani
CCM	Chama cha Mapinduzi
SEKTA YA KILIMO	Uzalishaji unaotokana na kilimo cha mazao ya biashara, mifugo, misitu na uvuvi
SEKTA YA VIWANDA	Uzalishaji unaotokana na machimbo uchimbaji, uzalishaji viwanda, umeme, usambazaji maji na ujenzi
SEKTA YA HUDUMA	Uzalishaji unaotokana na huduma za elimu, afya, sanaa, burudani, michezo, taarifa za makosa ya jinai na madai n.k.

SURA YA KWANZA

HISTORIA NA HALI HALISI YA DIASPORA ZANZIBAR

1.1 Utangulizi

Zanzibar ni Visiwa vilivyopo Afrika Mashariki katika Bahari ya Hindi vyenye wakaazi wenye asili kutoka maeneo tofauti duniani. Kama ilivyo desturi kwa watu wa visiwa, suala la kusafiri na kuhama ni utamaduni wao. Idadi kubwa ya watu wa Zanzibar kwa muda mrefu wamekuwa wakihamia sehemu mbali mbali za Tanzania Bara na nje ya Tanzania na kushiriki katika kutoa michango ya maendeleo kwa jamii. Kuna idadi kubwa ya Wazanzibari wanaoishi nje ya Tanzania (Diaspora) ambao kwa muda wote wamekuwa karibu na Nchi yao ya asili kwa kusaidia katika shughuli mbali mbali za maendeleo na kijamii.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikifanya juhudi mbali mbali katika kuwashirikisha Diaspora katika maendeleo ya Zanzibar. Katika miaka ya 1980, Mzee Ali Hassan Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Tatu aliwataka Wazanzibari waliopo nje (Overseas Zanzibari) kuja kuwekeza Zanzibar na kusaidia kufufua uchumi wake.

Aidha, katika miaka ya 1990, Mheshimiwa Dk. Salmin Amour Juma Rais wa Awamu ya Tano aliendeleza juhudi hizo kwa kuwataka Wazanzibari walioko nje kuja kuwekeza na kujenga nyumba za makaazi. Juhudi za hivi karibuni ziliendelea kufanyika ambapo Chama cha Mapinduzi (CCM) kiliamua kuliingiza suala la Watanzania wanaoishi ughaibuni katika Ilani yake ya Uchaguzi wa mwaka 2010 - 2015.

Ilani hiyo, Ibara ya 199 (j) CCM iliazimia kuendeleza mchakato wa kutambua Jumuiya za Watanzania wanaishi ughaibuni na kuweka utaratibu utakao wawezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao la asili.

Katika kutekeza ahadi ya Ilani ya CCM, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010, ilianza mchakato wa kuwashirikisha Wanadiaspora wa Zanzibar katika maendeleo. Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Saba alianzisha Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi ili iweze kuratibu shughuli za Wanadiaspora vizuri.

Tokea kuanzishwa kwake, Idara hii imefanya kazi ya kujenga uhusiano mwema kwa jamii ya Wanadiaspora na kuwashajilisha kushiriki katika Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii ya Zanzibar. Idara pamoja na mambo mengine imefanya ziara rasmi katika nchi za Oman, Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE), Brazil, India, Denmark na Ethiopia siyo tu kwa lengo la kuanzisha mahusiano rasmi na Wanadiaspora wanaoishi katika Nchi hizo, bali pia kujifunza kutokana na mifano mizuri ya kiutendaji kutoka Nchi hizo katika suala zima la utekelezaji wa dhana ya Diaspora.

Kwa upande mwengine Mapitio ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 ambayo yamelenga kuondoa umasikini uliokithiri na kufikia Maendeleo Endelevu yametambua mchango wa Diaspora katika maendeleo ya Zanzibar. Kwa sasa Mpango wa Muda wa Kati ni Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (2015-2020) umejumisha suala la Diaspora katika Mikakati ya Kimaendeleo na kupendekeza hatua za kuchukuliwa.

Hatua hizo ni pamoja na kutambua misaada ya kijamii ya Wanadiaspora kama mitaji ya maendeleo kwa Zanzibar, kutangaza Sekta za Uwekezaji kwa Wanadiaspora, kuhamasisha utalii kwa jamii ya Wanadiaspora na kuweka taratibu nafuu za kibenki kwa ajili ya Wanadiaspora.

1.2 Historia, Watu na Uchumi wa Zanzibar

Zanzibar ina eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 2,654; kati ya hizo kilomita za mraba 1,666 ni eneo la Kisiwa cha Unguja na kilomita za mraba 988 ni eneo la Kisiwa cha Pemba. Zanzibar imekuwa lango kuu la kibiashara kati ya Nchi za Mashariki ya Kati, India na Nchi nyengine za Afrika. Kabla ya karne ya 14, Wananchi wa Zanzibar walikuwa na utawala wao wa kujiendesha chini ya Mwinyi Mkuu. Inasadikiwa kuwa Mreno aliingia Zanzibar kati ya miaka ya 1498 na 1504 na kuanza kuitawala Zanzibar kwa takriban miaka mia mbili. Baada ya hapo, Sultani wa Oman aliitawala Zanzibar kuanzia mwaka 1698 hadi 1964. Zanzibar ilifanya Mapinduzi tarehe 12 Januari mwaka 1964 ambayo ndio yaliyoleta ukombozi kamili wa Wananchi wa Zanzibar. Baada ya Mapinduzi Matukufu, Zanzibar na Tanganyika iliyopata uhuru wake tarehe 9 Disemba, 1961 ziliungana tarehe 26 Aprili, mwaka 1964 na kuanzishwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hivyo, Mamlaka ya Serikali ya Tanganyika yaliingizwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilibakia na mamlaka ya kusimamia na kuendesha mambo yake yasiyo kuwa ya Muungano. Zanzibar ina mihimili yake mitatu ambayo ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Wawakilishi na Mahakama, isipokuwa Mahakama ya Rufaa ambayo imebakia kuwa ni Taasisi ya Muungano.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makaazi ya Tanzania ya mwaka 2012, idadi ya watu wa Zanzibar ni 1,303,569 ambayo inakua kwa asilimia 2.8 kwa mwaka. Asilimia 51.6% ya watu wa Zanzibar ni wanawake na asilimia 48.4% ni wanaume. Aidha, sensa hiyo ilibainisha kuwa asilimia 46.3% ya watu wa Zanzibar wanaishi vijijini na asilimia iliobakia wanaishi mijini. Idadi ya vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 35 ni asilimia 36.2% ya watu wote wa Zanzibar.

Takwimu za mwaka 2016, zinaonesha kuwa uchumi wa Zanzibar kwa kigezo cha pato la Taifa ni Shilingi za Kitanzania 2,628 Bilioni (kwa bei ya sasa). Idadi kubwa ya wananchi wa Zanzibar wanajishughulisha na kilimo cha kujikimu. Pato la mtu mmoja mmoja ni Shilingi za Kitanzania 1,806,000. Shughuli kuu za kiuchumi ni utalii, usafirishaji, mawasiliano, ujenzi, fedha na biashara.

Serikali inahakikisha kuwa mipango ya maendeleo na uwekezaji inaleta uwiano kati ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii. Mageuzi ya kiuchumi yaliyofanywa kuanzia miaka ya 1980, yameleta mafanikio makubwa katika kukuza uwekezaji binafsi kutoka ndani na nje hasa kwenye sekta za utalii, mawasiliano na usafiri. Takwimu zinaonesha kuwa uchumi wa Zanzibar unakua kwa kiwango cha kuridhisha; ambapo ulikua kwa asilimia 6.6% mwaka 2015.

1.3 Hali ya Diaspora Kimataifa

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Maendeleo ya Uchumi na Kijamii (UNDESA) limebainisha kuwa katika kipindi cha miaka hamsini iliyopita, idadi ya watu wanaoishi nje ya nchi zao za asili imeongezeka kutoka watu milioni 75 katika miaka ya 1960 hadi kufikia watu milioni 232, katika mwaka 2013; ikiwa sawa na asilimia 3% ya watu wote wa duniani.

Aidha, kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia ya mwaka 2011 inayohusu Diaspora kwa Maendeleo ya Afrika (Diaspora for Development in Africa) ilibainisha kuwa kiasi cha Waafrika milioni 30.6 wanaishi nje ya nchi zao za asili. Wanadiaspora hawa wamekuwa wakituma kiwango kikubwa cha fedha katika nchi wanazotoka zinazokadiriwa kufikia Dola za Kimarekani bilioni 40 kwa mwaka 2010 ambazo ni zaidi ya misaada ya kimaendeleo (ODA) na uwekezaji kutoka nje (FDI) zilizoingia katika nchi hizo kwa mwaka huo.

Taarifa rasmi ya Umoja wa Mataifa ya Mwaka 2015 imeeleza kwamba jumla ya wahamiaji wapatao milioni 230 walitarajiwa kutuma jumla ya US$ 500 bilioni kwenda katika nchi zinazoendelea katika mwaka 2015. Kutokana na kiwango hiki kikubwa cha utumaji wa fedha, Serikali za Nchi mbali mbali pamoja na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yameipa suala la Uhamiaji na Maendeleo umuhimu na mtazamo wa kipekee katika Sera na Mipango ya kiuchumi na kijamii.

1.4 Zanzibar na Hali ya Diaspora

Hakuna takwimu halisi wala taarifa sahihi ama za Watanzania au Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kama Diaspora kwa misingi ya idadi, sehemu walipo, umri, taaluma, mafunzo, kipato na uzoefu wao wa kitaaluma.

Taarifa ya Uhamiaji iliyotolewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mwaka 2015 inakadiriwa kwamba kiasi cha Watanzania 421,456 wanaishi nje ya nchi. Aidha, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kitabu chake cha "Zanzibar in Figure" cha mwaka 2015 kimeeleza kuwa kutokana na sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012 asilimia 1.2% ya Watanzania wanaishi nje ya nchi. Hata hivyo, takwimu hiyo haikuchambua idadi halisi ya Wazanzibari wanaioshi nje ya nchi.

Pamoja na tatizo hilo la kukosekana kwa idadi halisi ya Diaspora, kunajitokeza tatizo kama hilo la kukosekana kwa takwimu sahihi za kiwango cha fedha zinazotumwa na Wanadiaspora kuja Tanzania na Zanzibar kwa jumla. Kama ilivyodhihirishwa katika Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2013 kwamba ni vigumu kujua kiwango halisi cha fedha zinazotumwa na Wanadiaspora katika nchi zilizo chini ya Jangwa la Sahara. Benki Kuu ya Tanzania inakisia kuwa fedha rasmi zilizotumwa Zanzibar na Wanadiaspora kwa mwaka 2015 zilikuwa wastani wa Dola za Kimarekani 1.0 milioni.

Utaratibu wa kutumia njia zisizo rasmi katika kutuma fedha unaendelea licha ya kuwa baadhi ya Benki, ziliopo Tanzania Bara na Zanzibar zimeanzisha huduma maalumu za kutuma na kupokea fedha kutoka nje kupitia na kushirikiana na Western Union na Money Gram International. Imebainika kuwa ni Wanadiaspora wachache tu wa Zanzibar waliojitokeza kutumia huduma hizo rasmi. Hali hii inapelekea kukosekana kwa takwimu sahihi za fedha zinazotumwa na Diaspora kuja Zanzibar.

Inafahamika kwamba Zanzibar ina hazina kubwa ya Watu wenye asili ya Zanzibar ambao ni wataalamu, wasomi na mabingwa waliobobea wanafanya kazi katika Taasisi muhimu Barani Ulaya, Marekani, Canada na Mashariki ya Kati. Uwezo wa kitaaluma wa Wanadiaspora na utaratibu wa kuhamisha ujuzi walioupata kutoka nje ya nchi ni moja ya eneo muhimu la mchango wa Diaspora katika nchi wanazotoka na zile wanazoishi.

Kwa mfano katika mwaka 2013, Wanataaluma wa lugha ya Kiswahili wenye asili ya Zanzibar kutoka vyuo vikuu mbali mbali nje ya nchi wameshirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kuanzisha mitaala ya kufundishia Kiswahili

katika ngazi ya Uzamivu (PhD) na Uzamili (Post graduate). Wanataaluma hao pia wanapata fursa kuja kufundisha Kiswahili hapa Zanzibar kila mwaka. Mifano mingine ni pamoja na Chuo Kikuu cha Copenhagen nchini Denmark kilishirikiana na Wazanzibari walioko Denmark mwaka 2015 kuleta walimu kufundisha masomo mbali mbali katika Skuli tofauti ikiwemo Kisiwandui, Haile Selassie, Ben Bella na Nungwi. Katika sekta ya afya, Watanzania waliopo Marekani walileta madaktari wa fani tofauti kutoka ''African Women Cancer Awareness Association'' ambao walitoa mafunzo ya matibabu ya meno na utambuzi wa saratani za akina mama katika Zanzibar School of Health kilichopo Mombasa Zanzibar.

Misaada ya kijamii ya Wanadiaspora kwa kawaida inajuilikana kama mchango binafsi wa jamii ya Wanadiaspora kwa ajili ya kufanya mambo mbali mbali katika nchi zao za asili. Hakuna anayejua kiwango halisi cha mchango wa misaada ya kijamii kutoka nje katika shughuli za maendeleo ya Zanzibar. Hata hivyo, kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) ya mwaka 2010 inayohusu Matumizi ya Ulinzi wa Jamii, Mapitio ya Ufanisi na Bajeti ya Kijamii imebainisha kuwa misaada na michango iliyotolewa Zanzibar kwa misingi ya kidini inakisiwa kuwa ni asilimia 0.4% ya Pato la Taifa. Baadhi ya michango ya kijamii iliyotolewa na Wanadiaspora wa Zanzibar ni pamoja na vifaa tiba vilivyopelekwa Hospitali za Wilaya za Kivunge na Makunduchi na ujenzi wa Skuli ya Unguja Ukuu uliofanywa na Wazanzibari wanaoishi Canada.

Taasisi nyengine ya Diaspora ya Milele Foundation imetiliana saini mkataba wa makubaliano na baadhi ya Taasisi za Serikali katika utoaji wa misaada ya kijamii ikiwemo ujenzi wa Hospitali ya Welezo iliyopo Unguja, ujenzi wa matangi ya maji Makunduchi. Mfano mwengine mwaka 2015, Wanadiaspora wanaoishi nchini Seattle Marekani wamesaidia kukusanya viti

562 na meza 500 za kusomea ambazo baadae Serikali ilitoa fedha za kusafirisha kuja nchini. Vifaa hivyo vimesambazwa katika Skuli za Sekondari za Lumumba, Tumekuja na Mwanakwerekwe C kwa Unguja na Fidel Castro na Madungu kwa Pemba.

Sekta ya Utalii inachangia asilimia (80%) ya fedha za kigeni zilizokusanywa Zanzibar. Jamii ya Wanadiaspora wanaweza kuwa na umuhimu wa kufungua masoko mapya ya utalii na kuutangaza utalii katika nchi wanazoishi. Wanadiaspora wa Zanzibar wana uhakika zaidi wa kuzijua fursa na vivutio vya utalii vya Zanzibar kuliko wageni.

SURA YA PILI

MAANA YA DIASPORA WA ZANZIBAR, DIRA NA DHAMIRA YA SERA

2.1 Maana ya Diaspora

Neno Diaspora lina maana ya raia au mtu wa nchi moja anapoamua kuhamia nchi nyengine kwenda kuishi huko bila ya kupoteza uzalendo na upendo wa nchi yake ya asili. Mara zote mtu huyo hujengwa na mtazamo chanya katika harakati za maendeleo ya nchi yake ya asili.

Kwa madhumuni ya sera hii, Wanadiaspora wa Zanzibar ni Watu wenye asili ya Zanzibar wanaoishi nje ya nchi ambao wana uzalendo, wanatambua Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 kwamba yameleta ukombozi wa Watu wa Zanzibar na wanaheshimu Katiba na Sheria za nchi yao. Ni muhimu kwamba, watu hao wawe na hisia za kizalendo, hamu na ari ya kushiriki katika kuimarisha maendeleo ya Zanzibar. Uzalendo kwa mantiki ya Sera hii ni upendo wa nchi pamoja na harakati za kimaendeleo kwa kuzingatia Sheria na utulivu wa jamii bila ya ubaguzi.

Kwa mujibu wa Sera hii vigezo vikuu vya kumuwezesha mtu mwenye asili ya Zanzibar kutambulika kuwa Diaspora kwa ujumla ni vinne:-

a) Asili ya Zanzibar;
b) Uzalendo wa nchi;
c) Kutambua na Kuheshimu Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964; na
d) Utii wa Katiba na Sheria za nchi.

2.2 Miongozo ya Kanuni za Sera

Kufanikiwa kwa Sera ya Diaspora kumeunganishwa na miongozo mitano ifuatayo ya Kanuni za Sera:

i. Ushirikishwaji wa Wanadiaspora katika maendeleo ya Taifa.
ii. Kutambua umuhimu wa mchango wa Wanadiaspora katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
iii. Ushirikishwaji wa Taasisi na wahusika wote kwa kuunganisha juhudi zao katika mambo ya Diaspora kwenye utaarishaji wa Sera, utekelezaji, usimamizi na tathmini ya mikakati.
iv. Matumizi ya Takwimu sahihi za Diaspora katika kusimamia na kutathmini mafanikio ya utekelezaji wa Sera na Programu.
v. Kuzingatiwa kwa mahitaji ya kijinsia ili kutoa matarajio husika kwa jamii ya Diaspora wanaume na wanawake.

2.3 Dira ya Sera

Kuwa na jamii ya Wanadiaspora wenye uzalendo na moyo wa kuchangia na kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar.

2.4 Dhamira ya Sera

Kuwatambua, kuwaunganisha na kuwashirikisha Wanadiaspora wa Zanzibar katika umoja wao ili waweze kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya Zanzibar.

SURA YA TATU

HAJA YA KUWEPO KWA SERA NA MALENGO YAKE

3.1 Haja ya Kuwepo kwa Sera ya Diaspora

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua na inathamini Wanadiaspora wenye asili ya Zanzibar katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar. Zipo fursa nyingi ambazo ikiwa zitatumiwa vizuri zitasaidia katika kuharakisha maendeleo ya Zanzibar. Fursa hizo ni pamoja na misaada ya kifedha inayotolewa na Wanadiaspora kwa jamaa zao, uwekezaji, taaluma, ujuzi na teknolojia. Ili fursa hizi ziweze kutumika ipasavyo, kuna haja ya kuwepo kwa Sera ambayo itatoa muongozo kuhusu namna Wanadiaspora wa Zanzibar watakavyoshiriki katika kuleta maendeleo ya nchi yao ya asili.

Sera hii inajumuisha mambo muhimu na hatua mahsusi pamoja na mahitaji ya mfumo wa Sheria na Taasisi ambao utawekwa kuondosha changamoto zilizopo ili kuweza kuwashirikisha kikamilifu Wanadiaspora wa Zanzibar katika maendeleo ya nchi yao.

3.2 Malengo ya Sera ya Diaspora

i) Lengo kuu

Lengo kuu la Sera ya Diaspora ni kujenga mazingira mazuri yatakayowawezesha Wanadiaspora kushiriki na kuwafanya waweze kutoa mchango wao kwa maendeleo ya Zanzibar.

ii) Malengo mahsusi,

Sera ya Diaspora ya Zanzibar itazingatia hatua zifuatazo:

a. Kufanya mapitio ya Sera mbali mbali za kisekta ambazo zitaelezea na zitatoa maelekezo kuhusiana na masuala muhimu ya Diaspora na maendeleo ya Zanzibar;

b. Kuwashajihisha Wanadiaspora wote kushiriki katika maendeleo ya kijamiii na kiuchumi; na
c. Kuainisha fursa na wajibu wa Wanadiaspora wa Zanzibar.

SURA YA NNE

HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA

4.1 Kuijengea uwezo Idara inayoshughulikia masuala ya Diaspora

Hoja ya Sera:
Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Kuratibu Wazanzibari walioko Nje ya Nchi imeanzishwa mwaka 2010 na kupewa jukumu la kushughulikia masuala ya Wanadiaspora. Katika kipindi cha miaka saba, Idara inayoshughulikia Diaspora imeweza kuwakutanisha Diaspora katika maeneo mbali mbali duniani. Hali hii imeweza kujenga mafahamiano mazuri kati ya Wanadiaspora na Serikali. Hata hivyo, kutokana na suala la Diaspora ni lenye changamoto nyingi, Idara inayoshughulikia Wanadiaspora inahitaji kuongezewa uwezo.

Tamko la Sera:
Serikali itaimarisha Idara inayoshughulikia Diaspora kwa kuipatia nyenzo na wataalamu.

Mikakati ya Sera:

i. Kuwekeza katika kujenga uwezo wa kupata wataalamu;
ii. Kuipatia nyenzo za kutekeleza majukumu yake; na
iii. Kuiwezesha kuwa kituo kikuu cha taarifa za Diaspora.

4.2 Usimamizi wa Taarifa zinazohusu Diaspora

Hoja ya Sera:
Kupata taarifa sahihi za Diaspora ni moja ya jambo muhimu katika kupanga shughuli za kisera na maendeleo. Upatikanaji na usimamizi wa takwimu kamili na taarifa za uhakika za idadi ya Wanadiaspora, walivyotawanyika kijografia, kijinsia, ujuzi

na uzoefu, na pia utashi wao pamoja na uwezo wa Jumuiya zao ni jambo linalohitaji kuwekewa mkazo.

Tamko la Sera:
Serikali itaanzisha na kusimamia utaratibu maalum utakaoweka taarifa na takwimu za Wanadiaspora.

Mikakati ya Sera:

i. Kuwashajiisha Wanadiaspora kutoa taarifa zao sahihi na kufanya marekebisho kila inapohitajika;
ii. Kuandaa mfumo wa kielektroniki utakaowezesha kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kutafsiri taarifa na takwimu za Diaspora; na
iii. Kushirikiana na Taasisi nyengine za ndani na nje ya nchi ambazo zinaweka taarifa na takwimu za Diaspora ili kuleta uwiano mzuri.

4.3 Kuwashirikisha Wanadiaspora

Hoja ya Sera:
Kuwepo kwa utaratibu madhubuti wa kuwashirikisha Wanadiaspora kunarahisisha kujenga imani na kuimarisha mashirikiano kati yao na Serikali. Aidha, ushirikishwaji unajenga mfumo rahisi wa mawasiliano na kuaminiana.

Tamko la Sera:
Serikali itaanzisha mfumo madhubuti wa kuwezesha mashirikiano baina ya Serikali, Wanadiaspora na Taasisi nyengine zinazohusika.

Mikakati ya Sera:

i. Kuandaa mfumo wa kisheria na kitaasisi wa kuwashirikisha Wanadiaspora katika maendeleo ya Zanzibar;

ii. Kusimamia na kuendeleza Jukwaa la Diaspora kwa siku maalum ya Wanadiaspora;
iii. Kuongeza ufanisi wa matumizi ya Ofisi za Ubalozi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Jumuiya zao katika kuwashirikisha na kuwakutanisha.
iv. Kuweka utarabu wa kuimarisha mawasiliano na Jumuiya za Wanadiaspora ambazo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Ofisi za Ubalozi za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inaweza kushirikiana nazo;
v. Kuweka utaratibu sahihi wa kutoa habari kwa Wanadiaspora kupitia vyombo vya habari na tuvuti rasmi za Serikali;
vi. Kuwatumia Wanadiaspora kama Mabalozi wa kujenga ushawishi na utetezi katika kuelekeza maendeleo ya Zanzibar;
vii. Kujadiliana na Taasisi zinazohusika ili kuweka utaratibu maalum utakaohamasisha Wanadiaspora kushiriki katika maendeleo ya nchi yao; na
viii. Kutoa vitambulisho maalum kwa Wanadiaspora wenye sifa kushiriki ipasavyo katika maendeleo ya Zanzibar.

4.4 Kutumia Taaluma na Ujuzi wa Wanadiaspora kwa maendeleo ya Nchi

Hoja ya Sera:
Ujuzi na uwezo wa kitaaluma wa Wanadiaspora ni moja ya eneo muhimu la mchango wa Wanadiaspora katika nchi zao za asili. Kwa hivyo, kuna haja ya kuandaa utaratibu wa kuwawezesha Wanadiaspora kutumia ujuzi walioupata nje ya nchi.

Tamko la Sera:
Serikali itaweka utaratibu wa kuwawezesha Wanadiaspora kuutumia nchini ujuzi na taaluma waliopata wakiwa nje ya nchi kwa kuzingatia Sheria za nchi.

Mikakati ya Sera:

i. Kuwatambua Wanadiaspora wenye ujuzi na taaluma kwa mujibu wa mahitaji ya nchi;
ii. Kuandaa utaratibu utakaowavutia Wanadiaspora kuja nchini kwa lengo la kutumia ujuzi na taaluma zao; na
iii. Kuwapa fursa Wanadiaspora wenye sifa kushiriki katika zabuni mbali mbali kulingana na ujuzi na taaluma zao.

4.5 Utumaji Fedha kutoka kwa Wanadiaspora

Hoja ya Sera:

Wanadiaspora wengi wamekuwa na desturi ya kutuma fedha kwa jamaa zao kwa utaratibu usiokuwa rasmi. Utumaji wa fedha kwa njia za halali kutoka nje ya Nchi zinachochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Aidha, kuna fursa kwa Wanadiaspora kuweka akiba zao katika Benki za nchini na kuzitumia kama dhamana katika shughuli mbali mbali kama vile biashara na uwekezaji. Ni muhimu kuhamasisha matumizi ya mfumo ulio rasmi na nafuu katika utumaji na uwekaji wa fedha.

Tamko la Sera:

Serikali itazihamasisha benki kuandaa utaratibu utaowavuatia Wanadiaspora kutumia mifumo rasmi ya kutuma fedha kwa jamaa zao na uwekaji wa akiba.

Mikakati ya Sera:

i. Kuanzisha majadiliano na Benki Kuu kuhusu kuwepo kwa mfumo rasmi utakaowezesha Wanadiaspora kusafirisha fedha kihalali kuja Zanzibar kwa gharama nafuu na kufungua akaunti za akiba zitakaweza kutumika kama dhamana kwa shughuli za kibiashara na uwekezaji;

ii. Kujadiliana na Benki Kuu kuangalia uwezekano wa kurasimisha mfumo wa miamala ya fedha unaotumika na maduka ya kubadilisha fedha kwa Wanadiaspora; na
iii. Kuwashajihisha Wanadiaspora kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa hiari.

4.6 Diaspora na Biashara na Uwekezaji Vitega Uchumi

Hoja ya Sera:
Wanadiaspora wa Zanzibar waliopo ughaibuni na wale wanaorejea wanaweza kurahisisha ukuwaji wa pamoja wa biashara na uwekezaji kati ya nchi wanazoishi na nchi yao ya asili. Fursa za uwekezaji na biashara zilizopo ziwahamasishe Wanadiaspora kuzitumia kwa faida yao na kuwekeza kwa maendeleo ya Zanzibar.

Tamko la Sera:
Serikali itatangaza fursa zilizopo za uwekezaji kwa Wanadiaspora kupitia Taasisi zenye dhamana ya uwekezaji na Sheria zilizopo na kuweka vivutio vya uwekezaji vitakavyowashajihisha kuwekeza kupitia Ushirikiano wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na uwekezaji mwengine.

Mikakati ya Sera:
i. Kupitia Taasisi za uwekezaji na Ofisi za Ubalozi zetu, Wanadiaspora watapatiwa taarifa zote muhimu za fursa za uwekezaji na biashara;
ii. Kuandaa utaratibu maalum utakaowavutia Wanadiaspora kuwekeza Zanzibar;
iii. Kuwatangazia Wanadiaspora miradi ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kwa mujibu wa Sheria husika; na

iv. Kuwashajihisha Wanadiaspora kutumia taaluma na ujuzi walionao Wanadiaspora katika kuibua miradi mipya ya uwekezaji kupitia ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

4.7 Diaspora na Utalii

Hoja ya Sera:
Jamii ya Wanadiaspora inaweza kufungua masoko mapya ya utalii na kukuza biashara ya utalii katika nchi wanazoishi. Wanadiaspora wa Zanzibar wanaweza kutumika kama mawakala wa kuitangaza Zanzibar na vivutio vyake ili kuvutia watalii wengi zaidi kuja kutembelea nchi yetu.

Tamko la Sera:
Serikali itawatumia Wanadiaspora katika kuitangaza na kukuza biashara ya utalii wa Zanzibar.

Mikakati ya Sera:
i. Kuwapa habari na kuwaelimisha Wanadiaspora juu ya fursa na vivutio vya utalii vya Zanzibar;
ii. Kuwashajihisha Wanadiaspora wenye uwezo na ushawishi kufungua ofisi za uwakala wa kutangaza vivutio vya utalii viliopo Zanzibar ili kuwavutia watalii wengi zaidi; na
iii. Kuweka vivutio maalumu vitakavyowahamasisha Wanadiaspora kuja nyumbani kuzifaidi fursa za utalii zilizopo.

4.8 Diaspora na Misaada ya Kijamii

Hoja ya Sera:
Misaada ya kijamii kutoka kwa Wanadiaspora inaweza ikatumika kama chanzo kimoja wapo cha kupunguza umasikini

na pia sehemu ya mchango wa maendeleo kwa jamii. Kwa hivyo, ipo haja ya kuwepo mfumo wa kuratibu uletaji wa misaada ya kijamii kutoka kwa Wanadiaspora ili kutambua mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Tamko la Sera:
Serikali itaweka mfumo rasmi wa kuratibu misaada ya kijamii inayotolewa na Wanadiaspora ili kuhakikisha kuwa inaleta manufaa kwa wananchi.

Mikakati ya Sera:

i. Kuanzisha chombo kitakachoratibu mawasiliano, upokeaji na usambazaji wa misaada kutoka kwa Wanadiaspora;
ii. Kutambua mahitaji ya kijamii na kuyawasilisha kwa Wanadiaspora wenye dhamira ya kusaidia; na
iii. Kuhamasisha matumizi mazuri na uwekaji wa kumbukumbu za misaada na malengo yake.

SURA YA TANO

WAJIBU, MAJUKUMU YA KITAASISI, TATHMINI NA UFUATILIAJI

5.1 Mfumo wa Uratibu

Wahusika wote, ambao ni Serikali, Mawakala, Jumuiya za Wanadiaspora, sekta binafsi, Asasi za Kiraia na Jumuiya za Kimataifa wana majukumu ya kuhakikisha utekelezaji mzuri wa Sera ya Diaspora ya Zanzibar. Kwa hivyo, wahusika wote lazima wakati wote waoneshe utayari wa hali ya juu, ushirikiano na ari katika kuufuata utaratibu huu kwa madhumuni ya kuimarisha mashirikiano baina ya Serikali na Wanadiaspora.

Ufanisi wa uratibu ni muhimu kwa utekelezaji wa Sera na pia ni hatua muhimu inayohitajika katika kuimarisha ufuatiliaji na tathmini. Kwa sasa kazi za Diaspora zimegawanywa katika Wizara mbali mbali za Serikali, Idara na Mawakala. Bila ya shaka hali hii imesababisha kutawanyika kwa hatua za Kisera, kuingiliana majukumu na kutotumika vizuri rasilimali chache zilizopo. Uratibu wa pamoja wa mikakati ya Diaspora ni muhimu sana kwa ajili ya kuimarisha makubaliano ya pamoja kati ya wahusika na Taasisi za utekelezaji, kuondoa muingiliano wa majukumu na migogoro, kukuza ufanisi wa utekelezaji wa Sera na kutumia mashirikiano yaliyopo ya kitaasisi na wahusika wote.

5.2 Wajibu na Majukumu ya Kitaasisi

Kila Taasisi inayohusika moja kwa moja na utekelezaji wa Sera hii, majukumu yake yameainishwa katika Sura hii kama ifuatavyo:-

5.2.1 Idara inayoshughulikia Diaspora

Idara inayoshughulikia Diaspora itakuwa ni Taasisi kiongozi ya uratibu ya shughuli za masuala ya Diaspora na kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Itahakikisha kwamba Wizara, Idara na Mawakala wote wanaingiza masuala ya Diaspora katika Sera za kisekta na Programu zake;
ii. Itafanya kazi na Wizara, Idara na Mawakala wengine katika kuanzisha, kuendeleza na kuimarisha takwimu za Wanadiaspora wa Zanzibar pamoja na kuwa na mfumo madhubuti wa upatikanaji wa taarifa;
iii. Itaandaa viashiria vya ufuatiliaji na tathmini na kuviingiza katika Mfumo wa Taifa wa Ufuatiliaji na Tathmini;
iv. Itatoa muongozo wa Kisera kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Diaspora;
v. Itawatambua Wanadiaspora kupitia Jumuiya zao;
vi. Itahakikisha kuwa Wanadiaspora wenye sifa wanapewa vitambulisho maalum; na
vii. Itakuwa Sekretarieti ya Jukwaa la Diaspora.

5.2.2 Jukwaa la Diaspora

Jukwaa la Diaspora litakuwa na wajumbe kutoka Wizara, Idara, Mawakala wanaoshughulikia masuala ya Diaspora, Jumuiya za Wanadiaspora zinazokubalika Ubalozini kwetu, sekta binafsi na Washirika wengine muhimu. Jukwaa litaongozwa na Waziri anaeshughulikia masuala ya Diaspora. Jukwaa litakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuishauri Serikali juu ya masuala ya Diaspora; na
ii. Kufanikisha Kongamano na siku maalum ya Diaspora.

5.2.3 Majukumu ya Wizara, Idara na Mawakala wa Serikali na Wahusika wengine

Wizara, Idara, Mawakala wa Serikali wanaoshughulikia masuala ya Diaspora na Wahusika wengine watakuwa na majuku yafuatayo:-

i. Kurahisisha ushiriki wa Wanadiaspora katika shughuli za maendeleo kwa kufuata miongozo ya kisheria na kisera kwa ajili ya Wanadiaspora; na
ii. Kutoa taarifa za mahitaji ya Taasisi zao ambazo Wanadiaspora wanaweza kushirikishwa.

5.2.4 Tume ya Mipango

Tume ya Mipango itakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuhakikisha kwamba masuala yanayohusiana na Diaspora yanaingizwa katika Ajenda ya Maendeleo ya Taifa;
ii. Kuainisha maeneo ya uwekezaji wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi kwa Wanadiaspora; na
iii. Kuhakikisha kuwa Taasisi zote za Serikali zinahusisha Sera zao za Maendeleo na Programu kwa lengo la kuongeza mchango wa Diaspora.

5.2.5 Mamlaka Kukuza Uwekezaji Zanzibar

Mamlaka Kukuza Uwekezaji Zanzibar itakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira yatakayowezesha Diaspora kushiriki katika uwekezaji;
ii. Kuweka vivutio kwa ajili ya kuongeza ushiriki wa Wanadiaspora katika uwekezaji;
iii. Kutambua maeneo maalum kwa uwekelezaji kwa ajili ya Diaspora; na
iv. Kuwatumia Wanadiaspora katika kutangaza fursa za uwekezaji Zanzibar.

5.2.6 Benki Kuu, Benki za Biashara na Taasisi za Fedha

Benki Kuu, Benki za Biashara na Taasisi za fedha zitashajihisha kufanya yafuatayo:-

i. Kuweka mfumo wa kupunguza gharama za utumaji fedha kutoka nje; na
ii. Kuanzisha miamala ya kifedha kwa ajili ya Wanadiaspora.

5.2.7 Kamisheni ya Utalii

Kamisheni ya Utalii itakuwa na mjukumu yafuatayo:-

i. Itafanyakazi na Jumuiya za Wanadiaspora katika kuitangaza Sekta ya Utalii ya Zanzibar nje ya nchi;
ii. Kuwahamasisha Wanadiaspora kuwa Watalii katika nchi yao ya asili; na
iii. Kuwatumia Diaspora kufungua Ofisi za Mawakala katika nchi wanazoishi.

5.2.8 Jumuiya za Wanadiaspora wa Zanzibar

Jumuiya za Wanadiaspora wa Zanzibar zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuwahamasisha Wanadiaspora kujiunga katika Jumuiya zao;
ii. Kutambua jukumu lao la kusaidia maendeleo ya kiuchumi na kijamii;
iii. Kuitangaza Zanzibar na vivutio vyake katika uwekezaji na utalii katika nchi wanazoishi;
iv. Kuhamasisha Wanadiaspora kuwekeza Zanzibar na kuleta ujuzi na utaalamu wa teknolojia;
v. Kuwa na uhusiano wa karibu na Serikali na Ofisi za Kibalozi katika nchi wanazoishi; na
vi. Kutojihusisha katika ajenda nyengine zisiso na manufaa.

5.2.9 Washirika wa Maendeleo na Taasisi nyengine za Kimataifa

Washirika wa Maendeleo na Taasisi nyengine za Kimataifa watakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kusaidia kwa kuipa nguvu Serikali na washirika wengine katika kuendeleza azma ya Diaspora na Maendeleo; na
ii. Kubadilishana taarifa za Diaspora kwa msingi wa kuleta maendeleo.

5.2.10 Vyombo vya Habari

Vyombo vya Habari vitakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kujenga uelewa katika kuonesha mchango wa maendeleo wa Wanadiaspora kwa Zanzibar;
ii. Kuwaelimisha Wanadiaspora kuhusu shughuli za maendeleo; na
iii. Kudhibiti na kusahihisha upotoshaji wa taarifa unapotokea.

5.2.11 Ofisi za Kibalozi

Ofisi za Kibalozi zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuzitambua Jumuiya za Diaspora na Wanadiapora katika nchi wanazowakilisha;
ii. Kuwasaidia Wanadiaspora kuwapa taarifa za maendeleo za nchi yao ya asili; na
iii. Kuwa kiungo kati ya Wanadiaspora na nchi yao ya asili.

5.2.12 Idara ya Uhamiaji

Idara ya Uhamiaji itakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kutoa kipaumbele kwa Wanadiaspora kwa mahitaji ya vibali vya kuingia nchini; na
ii. Kuweka mazingira mazuri ya kutoa vibali vya kuingia nchini kwa Wanadiaspora.

5.3 Ufuatiliaji na Tathmini

Kwa kufikia malengo ya Sera hii, ni muhimu kuwa na muongozo mzuri wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini. Serikali itahakikisha kwamba Idara inayoshughulikia Diaspora itafanyakazi kwa bidii kuitekeleza Sera na kuhakikisha inafanyakazi na Washirika muhimu kwa ajili ya kuweka muda wa kufikiwa shabaha kwa kuanzisha miundombinu ya ufuatiliaji na tathmini. Malengo ya ufuatiliaji na tathmini yatajumuisha:-

(a) Kuwezesha mapitio ya utekelezaji wa Sera ya Diaspora, kwa upande wa rasilimali na upande wa matokeo, kutumia viashiria maalumu vitakavyoandaliwa;

(b) Kutoa mrejesho ambao utawezesha kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Diaspora; na

(c) Kuandaa mfumo shirikishi wa ufuatiliaji taarifa zilizotolewa kwa takwimu za kutosha kwa ajili ya kuandaa Sera.

Serikali itafanya mapitio ya Sera ya Diaspora kila inapohitajika.